



Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

HABARI JUU YA WANYAMAPORI KATIKA TANZANIA

**Wanyamapori kwa watanzania wote:
Kusimamisha upotevu, kuendeleza
raslimali na kupanua mafao**

KUHUSU MACHAPISHO HAYA

Kwanini wanyamapori?

Wanyamapori ni moja ya maliasili muhimu Tanzania. Kwakuwekamsingiwa utalii nchini, wanyamapori wana umuhimu wa kiuchumi. Ingawa serikali imewekeza vya kutosha, wanyamapori wameendelea kupungua kwa nchi nzima kama zinavyoonesha takwimu. Kupungua kwa wanyamapori kutaendelea kujitokeza mahali mahali kwa vile idadi ya watu imeongezeka mara nne tangu wakati wa uhuru na hivyo ardhi zaidi inatakiwa kwa ajili ya kilimo na matumizi mengine. Hata hivyo watu wengi wanafikiria kupungua kwa wanyamapori kunahusishwa na mfumo uliopo wa usimamizi wa wanyamapori. Na mapungufu hayo yamesababisha kutofikia malengo ya kugawanya mafao ya kiuchumi kitaifa na katika jamii, kukosekana kwa uwekezaji katika wanyamapori, migogoro baina ya mahitaji ya jamii na sera za uhifadhi, na hatimaye kupungua kwa idadi ya wanyamapori.

Machapisho haya ya kisera yanalenga kutoa mapendekezo ya kujenga juu ya jinsi uwekezaji unaovutia kwa serikali ya Tanzania na jamii katika uhifadhi wa wanyamapori uboreshwe ili kuwa endelevu, wenye haki na matokeo yenye manufaa. Ni kwa vipi wanyamapori wanaweza kuwa na faida kwa kila mtanzania hasa watanzania waishio vijijini ambako maisha ya wanyamapori yanategemea?

Machapisho haya ni kwa ajili ya nani?

Machapisho haya yameandaliwa kama vitini kwa ajili ya watunga sera na umma kwa ujumla ambao wanataka habari katika sekta ya wanyamapori. Machapisho

haya yanatoa habari, takwimu, na uchambuzi yakinifu juu ya mwelekeo na idadi ya wanyamapori Tanzania, sababu za mwenendo huo na uhusiano wa ukuaji wa uchumi kitaifa, kupunguza umaskini, na usimamizi wa wanyamapori. Lengo la habari ni kuhimiza mjadala uliojuvywa juu ya sera na desturi zinazosimamia wanyamapori katika Tanzania.

Je, machapisho haya yana uwiano sawa na ni yenye haki?

Kila jitihada imefanyika ili kuanzisha uchambuzi wenye uwiano sawa juu ya masuala kwa kutegemea takwimu na habari zilizopo. Utalii wa uwindaji na ule wa picha, vyama hiari (mashirika ya kijamii, mashiriki yasiyo ya kiserikali nchini, na yale ya kimataifa), serikali (Idara ya Wanyamapori) na watalaam wa kujitegemea wote wamehusishwa katika uandaaji wa machapisho haya. Kila jitihada imefanyika ili kutokuhimiza matakwa ya mtu au kikundi binafsi dhidi ya wengine – kila mmoja ana nafasi katika usimamizi na kufaidika kutokana na wanyamapori Tanzania!

Kuchimbua zaidi kutokana na machapisho haya

Muhtasari wa mapitio mwanzoni mwa machapisho haya unatoa habari muhimu na mapendekezo ya kisera kwa ufupi. Baada ya hapo machapisho yamepanywa kwa mfuatano wa mada kwa maeneo makuu ya sekta ya wanyamapori. Orodha ya vyanzo vya habari na kujifunza zaidi vimewekwa.

Kwa kushirikiana na



© JMT 2008